



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

Afya Halisi



Mahojiano na wahudumu wa huduma ya dhuluma za kijinsia (Kituo)

Tarehe y: a mahojiano	Saa ya kuanza: Saa ya kumaliza:
Jina la anayehoji:	Jina la anayechukua matini:
Kaunti:	Kaunti mdogo/mtaa:
Jina la taasisi/shirika:	Jina la anayehojiwa:
Nafasi ya anayehojiwa:	Anwani ya anayehojiwa: Simu: Barua pepe:

Matini ya mwezeshaji:

- Kabla ya kuanza, Mwezeshaji ahakikishe fomu zote za wale watakaoshiriki zimewekwa sahihi.
- Kundi likiwa tayari, kabla ya mahojiano kuanza, mwezeshaji lazima aambie kikundi: Jina langu ni _____ na ninafanya kazi na mradi wa Afya Halisi. Ahsante kwa muda wako wa kuzungumza na sisi leo. Nataka kuchukua muda kuongea na wewe leo kuhusu huduma za GBV. Mwenzangu, _____ ako hapa kunisaidia kuchukua matini . Kushiriki kwako mazungumzo ya leo ni kwa hiari. Unaweza kujiondoa wakati wowote .Hutapoteza manufaa yoyote ikiwa hutashiriki. Vile vile hutapata manufaa ya ziada ikiwa utashiriki. Chochote tutazungumza hapa leo ni siri. Hakuna chochote utasema kitahusishwa na jina lako. Mazungumzo yasisizi masaa mawili. Kabla tuanze, una maswali yoyote ?
- Jibu maswali yote, alafu uliza, Unaweza kuendelea ?
- Mruhusu yeyote ambaye hangependa kuendelea, alafu anza mahojiano. Melezo ya upeanaji huduma

I. Melezo ya upeanaji huduma

- Ni huduma zipi za FP/RMNCAH ambazo zinapatikana kituoni kwa sasa ?
- Wateja wako kimsingi ni kina nani ? (Dokeza wanawake, wanaume, wanarika. Sababu yah ii unafikiria ni nini ?
- Ni huduma zipi dhidi ya dhuluma za kijinsia ambazo zinapeanwa kwa sasa hapa kituoni ? Nani huzipeana ? (dokeza: wahudumu ni wa kike au wa kiume ?) Rufaa zinatolewa kwa mambo yasiyo ya kliniki ?

II. Mitazamo ya kitamaduni kuhusu dhuluma za kijinsia

- Watu katika jamii hii wanafikiriaje kuhusu dhuluma za kijinsia ? Hii ni tofauti aje kwa wanawake na wanaume ?

2. Ni aina gani ya dhuluma za kijinsia ambazo hupatikana sana ? Nani ameathirika sana ? (*kama haijatajwa, dokeza kuhusuFGM/C na ubakaji*)
3. Ni zipi baadhi ya imani, tamaduni, au mitazamo katika jamii hii ambayo inaongeza dhuluma za kijinsia ?
4. Kwa maoni yako, ni kwa kiasi gani vijana waliobaleghe na watu wadogo katika jamii hii wako katika hatari ya dhuluma za kijinsia ? (*Dokeza: ni zipi baadhi ya tamaduni na mambo ya kijamii ambao huzidisha hatari ya dhuluma za kijinsia ?*)
5. Ni changamoto zipi waathiriwa wa dhuluma za kijinsia hupitia katika jamii hii ambazo huwafanya wasitake kuripoti ? Au kuifanya vigumu kwao kupata huduma ? (*Dokeza changamoto zinazohusiana na mitazamo, unyanyapaa wa jamiiu, kufikia rasilimali na huduma,maeneo salama*)
6. Ni vipi washawishi wa jamii hujibu dhuluma za kijinsia katika jamii:
 - a. Wanachukuliaje kesi za ubakaji ?
 - b. Wanachukuliaje kesi za ubakaji wa watoto wadogo ?
 - c. Wanachukuliaje kesi za vita ?
 - d. Wanachukuliaje kesi za FGM/C ?

III. Upeanaji wa huduma dhidi ya dhuluma za kijinsia

1. Ni huduma zipi za kiafya ambazo zinapatikana kwa sasa kwa waathiriwa wa dhuluma za kijinsia ambao wanakuja katika kituo hiki ?
2. unahakikisha aje waathiriwa wa dhuluma za kijinsia, wa jinsia au umri wowote, wanashughulikiwa kwa ufaragha ? Kuna tofauti kwa waathiriwa waliobaleghe ?
3. Ni mambo yapi yamezingatiwa kuhakikisha umakini katika kutoa huduma dhidi ya dhuluma za kijinsia ?
4. Ni nini inafanywa kijamii kuwatia watu moyo wa kutafuta huduma zinazohusiana na dhuluma za kijinsia katika kituo hiki ? Nani huzitekeleza ? Mara nyingi aje ? Ni nani wanalengwa ?
5. Kuna mikakati ya kituo/au kijamii community ambayo inatekelezwa kuwasaidia waathiriwa wa dhuluma za kijinsia kupata huduma kwa wakati unaofaa
6. Ni vizuizi vipi vya upeanaji huduma ambavyo huwafanya waathiriwa kutotafuta huduma dhidi ya dhuluma za kijinsia ? (*dokeza kuhusiana na gharama, wakati wa kufanya kazi, mitazamo ya huduma*) kituo hiki kinayashughulikia vipi haya ?
7. Ni mikakati ipi kituo kimeweka ili kushughulikia mahitaji ya vijana waliobaleghe wanaokumbwa na dhuluma za kijinsia ?
8. Wahudumu wanahisi vipi kupeana huduma dhidi ya dhuluma za kijinsia ? Wako sawa na kiwango chao cha mafunzo ? Wako na bidhaa vyote wanavyohitaji ? Wako sawa kushughulikia wateja Fulani kuliko wengine ?
9. Ni kada gani ya wahudumu ambayo imepokea mafunzo jinsi ya kuwahudumia waathiriwa wa aina yoyote ya dhuluma za kijinsia ? (*Dokeza: kwa aina ya dhuluma za kijinsia ambayo imetajwa hapo juu*) Ni mafunzo yapi yanahitajika ?
10. Ni mashirika gani pia hutoa huduma dhidi ya dhuluma za kijinsia katika jamii hii ? Mnashirikiana vipi na wao ?
11. Kuna chochote ungependa kutuambia ?

Matini ya mwezesaji:

- Baada ya swali la mwisho kuulizwa, ambia (wa) mshiriki: Tumefika mwisho wa mahojiano yetu. Kabla tufunge, una maswali yoyote ya mwisho kwangu ?
- Jibu maswali yaliyobaki, alafu washukuru washiriki kwa muda wao.
- Waeleze washiriki ikiwa kuna chochote wanaitaji kufanya ili kupata malipo yao ya nuli na mambo mengine ya kiofisi